**HOTUBA YA MHESHIMIWA CHARLES MAKONGORO NYERERE MKUU WA MKOA WA RUKWA ALIYOITOA KWENYE KIKAO CHA BARAZA LA MADIWANI LA HALMASHAURI YA WILAYA YA NKASI KUHUSU UTEKELEZAJI WA HOJA ZA UKAGUZI NA MAPENDEKEZO YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA MWAKA 2022/2023 KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI TAREHE 24 JUNI, 2024.**

- ***Katibu Tawala wa Mkoa,***
- ***Mheshimiwa Mwenyekiti wa Halmashauri,***
- ***Ndugu Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya,***
- ***Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Nkasi,***
- ***Waheshimiwa Madiwani,***
- ***Kamati ya Usalama ya Wilaya,***
- ***Mkaguzi Mkuu wa Nje wa Mkoa kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,***
- ***Wataalam kutoka Sekretarieti ya Mkoa,***
- ***Katibu Tawala wa Wilaya ya Nkasi,***
- ***Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri,***
- ***Wataalamu wa Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi,***
- ***Maafisa Tarafa,***
- ***Wageni Waalikwa,***
- ***Waandishi wa Habari,***
- ***Mabibi na Mabwana.***

**Nawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania………… Kazi Iendelee.**

***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Awali ya yote napenda nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia sisi sote kuwa na afya njema. Kwa namna ya pekee nimshukuru na kumpongeza **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa namna anavyoiongoza nchi yetu kwa weledi mkubwa na kuitangaza nchi yetu Kimataifa. Namshukuru **Mh. Dkt. Samia Suluhu Hassan** kwa kuendelea kuniamini na kuniteua kuwa Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Aidha nimshukuru sana kwa kutuletea fedha nyingi kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo ya Wananchi kwenye Sekta za Afya, Elimu, Miundombinu ya Barabara, na Maji.

***Msheshimiwa Mwenyekiti,*** Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi katika mwaka huu wa Fedha imepata Hati Inayoridhisha. Nitumie fursa hii kukupongeza wewe pamoja na Waheshimiwa Madiwani, Mkurugenzi pamoja na Wataalamu wote kwa kupata Hati Inayoridhisha. Naomba ushirikiano huu kati ya Waheshimiwa Madiwani pamoja na wataalamu uendelee ili kuhakikisha kuwa mnaendelea kupata Hati Inayoridhisha kwa mwaka huu na miaka ijayo.

***Msheshimiwa Mwenyekiti,*** Naomba sasa nizungumzie uchambuzi wa taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023 hususani katika maeneo ya msisitizo kwa Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi kama ifuatavyo:

***Mheshimiwa Mwenyekiti*****,** Katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2022/2023 iliyotolewa April, 2024 ilionyesha kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi ilikuwa na Hoja za miaka ya nyuma ambazo hazijafungwa **26** na Hoja za Mwaka huu (2022/23) ni **24** hivyo kufanya Jumla ya Hoja **50**. Pia Halmashauri ilikuwa na jumla ya maagizo sita (4) ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) ambayo hayajatekelezwa hadi sasa. Natambua Katibu Tawala Mkoa kupitia barua na vikao mbalimbali amesisitiza juu ya kujibu Hoja hizi na kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo katika utekelezaji wa shughuli za Serikali ili kuepuka kuzalisha hoja zisizo za msingi. Kupitia Kikao hiki nikutake Mkurugenzi na Wataalam wako kushirikiana na Mkaguzi Mkuu wa Nje kuhakiki Hoja hizi ili zijibiwe kufungwa na kuhakikisha kuwa **maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za mitaa (LAAC) yanatekelezwa**

**ipasavyo**. Pamoja na Hoja hizi zipo Hoja ambazo ningependa kusisitiza hapa ambazo Halmashauri yako inatakiwa kuzifanyia kazi kwa haraka;

1. Kuhusu Usimamizi wa Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani, Mkaguzi amebainisha maeneo ambayo Halmashauri haifanyi vizuri katika Ukusanyaji wa mapato ikiwemo Mapato ya Kiasi cha **Shilingi 85,156,600** ambayo yamekusanywa lakini hayajawasilishwa Benki, nikutake Mkurugenzi kuweka mikakati ya kuhakikisha Halmashauri inakusanya mapato kikamilifu lakini pia kuhakikisha fedha zote zinazokusanywa zinawasilishwa Benki kwa wakati kama Sheria za Fedha zinavyoagiza. Natambua Katibu Tawala Mkoa kupitia Barua ya **tarehe 10 Juni, 2024** amekwishatoa maelekezo ya marufuku ya kutumia fedha mbichi na kuchukua Hatua Stahiki za kinidhamu na kisheria dhidi ya Watumishi waliotumia fedha mbichi na kufanya udanganyifu au hujuma ya mapato ya Halmashauri, nami **nasisitiza ni marufuku kutumia fedha mbichi na wote waliohusika wachukuliwe hatua stahiki za kinidhamu na kisheria.** Vile vile katika ufuatiliaji uliofanywa na Mkoa umebaini kuwa yapo mapato katika Mfumo wa TAUSI yaliyokusanywa na Watendaji wa Halmashauri **kiasi cha Shilingi 53,638,830** ambayo hayajawasilishwa benki mpaka tarehe 21 Juni 2024. Nikuagize tena Mkurugenzi kuchukua Hatua Stahiki kuhakikisha Fedha hizo zinarejeshwa na Wahusika wanachuliwa Hatua za kinidhamu na kisheria kwa kuzingatia **Kanuni ya 36 - 37 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za Mwaka 2022.**
2. ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Mkaguzi katika Taarifa yake amebaini kuwa Halmashauri yako imeshindwa kukusanya mapato kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwemo kiasi cha **Shilingi 14,659,500** kutoka chanzo cha uchinjaji na ukaguzi wa nyama, kiasi cha **Shilingi 11,800,000** kutoka kwenye kodi ya pango**,** dosari hizi zimeendelea kuzorotesha ukusanyaji wa mapato na hivyo halmashauri yako kushindwa kufikia malengo ya ukusanyaji mapato kulingana na makisio. Nimearifiwa kuwa mpaka Tarehe 21 Juni, 2024 (Ijumaa)

Halmashari yako ya Nkasi ilikuwa imekusanya kiasi cha **Shilingi 2,335,070,005.97** sawa na **asilimia 75%** ya kiasi cha **Shilingi 3,133,755,000.00** ambayo ilikasimiwa kwa Mwaka wa fedha 2023/24.Ni dhahiri kuwa Halmashauri haitafikia lengo la makusanyo ya mapato ya ndani kwa mwaka huu wa fedha. Mwenendo wa ukusanyaji unaonesha kuwa Halmashauri imekuwa inashuka katika asilimia za ukusanyaji kwa muda wa miaka mitatu mfululizo kama ifuatavyo;

| Mwaka wa fedha | Makisio ya mapato | Hali halisi kilichokusanywa | Asilimia |
|---|---|---|---|
| 2021/2022 | 2,743,267,799 | 2,438,226,553 | 89% |
| 2022/2023 | 3,010,391,707 | 2,507,890,530 | 83.3% |
| 2023/2024 | 3,133,755,000 | 2,335,070,005.97 | 75% |

Kutokana na mwenendo huu usioridhisha wa ukusanyaji wa mapato; **Nikuagize Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya kuunda timu ya wataalamu kuchunguza eneo la ukusanyaji na usimamizi wa mapato katika Halmashauri hii.** Uchunguzi huu uhusishe Pamoja na mambo mengine, namna vyanzo vinavyoibuliwa, takwimu za vyanzo vya mapato vilivyopo (revenue collection data base), namna ukusanyaji unavyofanyika na kama fedha zote zinawasilishwa benki kwa wakati na taratibu za kuwalipa wakusanyaji. Taarifa ya timu hiyo ya watalaamu inifikie ofisini kabla ya tarehe 25 Julai, 2024.

3. **Eneo la Ununuzi na Usimamizi wa Miradi,** katika taarifa ya CAG, imeonekana Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi ina Udhaifu katika uzingatiaji wa Sheria ya Ununuzi wa umma ya mwaka 2011 kama ilivyorejewa mwaka 2016 pamoja na Kanuni zake za mwaka 2013 na 2016 pamoja na usimamizi wa Mikataba ya miradi. Dosari hizi alizobaini Mkaguzi pamoja na mambo mengine zinazorotesha jitihada za Serikali katika utekelezaji wa Miradi na kuwaletea Wananchi maendeleo, kwa tathmini yangu mapungufu mengi katika miradi yanatokana na eneo hili la Ununuzi na usimamizi hafifu wa miradi, hivyo Halmashauri inapaswa kutilia mkazo katika eneo hili. Kwa kuzingatia matumizi ya Mfumo wa Ununuzi (NeST) na kukiimarisha

Kitengo cha Ununuzi. Aidha Menejementi yote ya Halmasahuri inatakiwa kuhakikisha inatekeleza majukumu kwa kuzingatia Sheria, Taratibu na Kanuni za Ununuzi ili kuepusha Hoja. Baadhi ya Hoja katika eneo la Ununuzi na usimamizi wa Miradi zilizobainishwa katika Taarifa CAG ni pamoja na: -

a) Mapungufu mbalimbali katika miradi inayotekelezwa kwa njia ya "***Force Account"*** kwenye Shule za Milundikwa Sekondari, Kate, Mashete, Myula, Isale na Zahanati ya Tambaruka;
b) Kutokukamilika kwa Miradi iliyopokea fedha kutoka mradi wa ***BOOST*** iliyokuwa inatekelezwa kwenye Shule za Msingi Isaba, Ntalamila na Mtakuja;
c) Kutotumia nyaraka rasmi za utangazaji wa zabuni (tendering document) na hati msako (**Quotations)** zinazotolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) kwa Ununuzi wenye thamani ya **Shilingi 736,625,295**;
d) Mapungufu mbalimbali kwenye Hati msako/Kotesheni za Ununuzi za **Shilingi 94,093,131;**
e) Ununuzi uliofanyika kwa fedha taslimu kiasi cha **Shilingi 117,429,000 na;**
f) Mapungufu mbalimbali katika malipo yaliyofanyika kwa Wazabuni yenye thamani ya **Shilingi 40,530,932.**

Ni dhahiri eneo hili linaitia dosari Halmashauri na kuendelea kufifisha juhudi za Serikali katika kukamilisha Miradi kwa thamani ya Fedha inayotolewa. Nakuagiza Mkurugenzi kuchukua hatua stahiki kurekebisha kasoro zote zilizojitokeza. Kuhakikisha Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi kinatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sheria na Taratibu za Ununuzi, Matumizi ya Mifumo na kuwachukulia hatua watumishi wote wa Halmashauri (ngazi ya chini na makao makuu) waliosababisha hoja hizi za ununuzi zenye viashiria vya uzembe, kutotimiza wajibu, na kutozingatia Sheria.

4. Matumizi ya Mifumo mbalimbali, ***Msheshimiwa Mwenyekiti,*** Serikali imeendelea kufanya maboresho ya Mifumo mbalimbali ikiwemo

mfumo wa kukusanyia mapato (TAUSI), Mfumo wa kusimamia mali za Serikali (GAMIS), Mfumo wa Mipango/Bajeti na Taarifa (PLANREP) pamoja na mifumo mingine ya fedha na utawala, Mkaguzi amebainisha mapungufu mbalimbali katika matumizi ya mifumo hiyo. Nikuagize Mkurugenzi kwa kushirikiana na Wataalam kuhakikisha kasoro zote zilizobainishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zinarekebishwa na mifumo hiyo inatumika kikamilifu.

5. **Usimamizi wa Mali za Halmashauri;** Mkaguzi katika Taarifa yake alibainisha uwepo kwa Boti Mbili zenye thamani ya **Shilingi 99,915,320** ambazo hazikupokelewa kutokana Mzabuni aliyezileta kutokamilisha baadhi ya matakwa ya Kimkataba, pamoja na kuwasilisha utekelezaji wa jambo hili kwa CAG nakuagiza uwasilishe Taarifa ya Utekelezaji kwa Katibu Tawala Mkoa ukirejea barua yake ya **Tarehe 2 Mei, 2024** na maelekezo niliyoyatoa kwenye Kikao cha Kudhibiti na Kusimamia Mapato na Matumizi ya Mkoa kilichofanyika **Tarehe 24 Mei, 2024.**
6. **Uwepo wa Mashauri ya kesi na Madeni ya Halmashauri;** Mkaguzi kwenye taarifa amebainisha mapungu mbalimbali kwenye eneo hili, mfano Halmashauri yako ina mashauri kwenye mabaraza na Mahakama yenye thamani ya **Shiligi 71,483,911,** Deni la Mfuko Wa Hifadhi ya Jamii **Shilingi 60,762,082,** na Madeni mbalimbali ya watumishi na Wazabuni yenye thamani ya **Shilingi 1,350,576,190.** Nikuagize Mkurugenzi simamia wataalamu wako, dosari hizi zinachafua taswira ya Hamashauri, Mkoa na Serikali kwa ujumla.
7. **Udhaifu katika utekezaji wa Bajeti**, *Mkaguzi kwenye katika Taarifa yake amebani yafuatayo;* Mapungufu katika upelekaji wa asilimia 40 ya Mapato ya Ndani kwenye Miradi ya Maendeleo ambapo CAG katika Taarifa yake amebaini kuwa Halmashauri ya Nkasi haikupeleka kiasi cha **Shilingi 225,241,998** cha Mapato ya Ndani kwenye Miradi ya Maendeleo. Nikuagize Mkurugenzi kuhakikisha kuwa Matumizi yote yanayofanyika yanazingatia sheria ya Bgajeti

Na.11 ya mwaka 2015 na miongozo ya bajeti iliyowekwa na siyo vinginevyo.

8. **Mheshimiwa Mwenyekiti;** Mkaguzi pia amebaini mambo kadhaa na kuyaanisha kwenye Taaria yake kama ifuatavyo;

    i. Kutoa fedha pungufu kwa ajili shughuli za lishe kiasi cha **Shilingi 61,460,000;**
    ii. Bakaa ya Fedha za Ununuzi wa Boti zilizotumika kwa matumizi mengine kiasi cha **Shilingi 128,080,000;**
    iii. Kutenga fedha pungufu kwa ajili ya ulipaji wa madeni kiasi cha **Shilingi 1,350,576,190;**
    iv. Upotevu wa mapato kutoka Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kutokana na mapungufu katika uwasilishaji wa madai kiasi cha **Shilingi 37,340,295 na;**
    v. Kuchelewa kuwasilisha Taarifa za Hesabu za Mwisho kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kinyume na Waraka wa Katibu Mkuu Hazina na Mlipaji Mkuu wa Serikali Na. 3 wa mwaka 2022/23.

Nikuagize Mkurugenzi kurekebisha Dosari hizi ambazo Mkaguzi amebainisha kwenye Taarifa yake.

***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Pamoja na maelekezo niliyoyatoa wakati wa uchambuzi wa hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali naomba nitoe maelekezo ya jumla kwa Halmashauri yako ili kupunguza na kuepuka Hoja za Ukaguzi kama ifuatavyo: -

i. Nasisitiza hatua stahiki za kinidhamu na kiutumishi zichukuliwe kwa watumishi wote ambao wameonekana kusababisha hoja kutokana na uzembe bila kumuonea mtu kwa kufuata taratibu na Kanuni za utumishi wa umma za mwaka 2022, taarifa hii iwasilishwe Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kabla ya Tarehe 26 Juni, 2024.

ii. Kutoa ushirikiano kwa Wakaguzi wa Nje pindi wanapofanya Ukaguzi badala ya kusubiri Hoja za Ukaguzi kutolewa, Vilevile Wakuu wa Divisheni na Vitengo husika wahusike kikamilifu kutoa ufafanuzi kwa Wakaguzi badala ya kuwatumia Wasaidizi wakati wa zoezi la

ukaguzi. Hii itasaidia baadhi ya Hoja kuisha wakati Ukaguzi ukiendelea.

iii. Kuimarisha mifumo ya Udhibiti wa ndani (Internal control systems), kuimarisha Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani, Kitengo cha Fedha, na utendaji kazi wa Kamati ya Ukaguzi (Audit committee).

iv. Halmashauri iimarishe eneo la usimamizi wa Ununuzi kwa kuhakikisha Sheria na Taratibu za Ununuzi zinafuatwa kikamilifu. Na kwa sasa Sheria mpya ya ununuzi wa umma ya mwaka 2023 na kanuni zake za mwaka 2024 zimeanza kutumika tarehe 17 Juni, 2024. Hivyo kwa miradi itakayotekelezwa kwa njia ya "Force Account" hakikisheni kabla ya ununuzi kufanyika katika miradi ya maendeleo kuwepo kwa mchanganuo wa gharama (schedule of requirements/materials) ili kutoruhusu ununuzi holela wa vifaa au zaidi ya mahitaji.

v. Kuimarisha na kusimamia matumizi ya mifumo mbalimbali ikiwemo mfumo wa Ununuzi wa umma (NeST), Mfumo wa kukusanyia Mapato (TAUSI), Mifumo ya Malipo (MUSE na FFARS).

vi. Utekelezaji wa maelekezo haya pamoja na kuwasilisha mpango wa utekelezaji wa Hoja uwasilishwe Ofisini kwangu kabla ya tarehe 26 Juni 2024 ili taarifa hizi ziunganishwe na kutumwa TAMISEMI kabla tarehe 30 Juni 2024.

***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Mwisho, Napenda kukushukuru tena wewe pamoja na Waheshimiwa Madiwani na timu ya Menejimenti ya Halmashauri kwa kunialika kuhudhuria kwenye kikao hiki muhimu. Aidha katika zoezi la uandikishaji wa wapiga kura litakaloanza Julai kwa ajili ya uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 nawasihi Waheshimiwa Madiwani hamasisheni Wananchi kujitokeza kwa wingi ili mwakani watumie haki yao ya Kidemokrasia. Nawakumbusha pia kuwa mwaka huu 2024 kutakuwa na uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Nawaomba tuwahamasishe wananchi kujitokeza kuchagua viongozi wao muda utakapofika.

Mungu Ibariki Tanzania,

Mungu Bariki Mkoa wetu wa Rukwa,

Mungu Bariki Halmashauri ya Nkasi.

Asanteni sana kwa Kunisikiliza.

Mhe. Charles Makongoro Nyerere

**MKUU WA MKOA RUKWA**